

Ni siri gani zilizofunuliwa kwa kufunguliwa kwa mihuri saba?

Mathayo Mt 13:10-17

“Wakaja wanafunzi wakamwambia kwa nini wasema nao kwa mifano? Akajibu akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa. Kwa maana yoyote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele, lakini yeyote asiye na kitu hata kile alichu nacho atanyang'anywa. Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano kwa kuwa wakitazama hawaoni na wakisikia hawasikii, wala kuelewa. Na Neno la Nabii Isaya linatimia kwao, likisema,

Kusikia mtasikia wala hamtaelewa; kutazama mtatazama, wala hamtaona. Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao wakasikia kwa masikio yao; wakaelewa kwa mioyo yao, wakaongoka, nikawaponya. Lakini heri macho yenu kwa kuwa yanaona; na masikio yenu kwa kuwa yanasikia. Kwa maana amin nawaambia, manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi wasiyasikie”
Ufunuo 10:7.

“Isipokuwa katika siku za malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii”

Angalia! Kile kilichokuwa mwanzoni siri kubwa ya Mungu, usiri mkubwa wa siri ya Mungu iliyokuwa katika nia yake, sasa hivi imewekwa kwenye mioyo ya waamini, ambao ni mwili wa Kristo kile kilichokuwa ni siri kuu ya Mungu katika Nia yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu sasa hivi kimedhihirishwa fikiria hilo! Ninauhakika hatulipati hilo vema, silioni nipaswavyo kuliona pia, na nina uhakika hamlioni. Lakini ile siri kuu ya Mungu, kile Mungu wa milele alichokuwa nacho kama siri, imewekwa wazi sasa ndani ya Yesu Kristo, halafu ikatolewa lipewe kanisa lake. Kile

kilichokuwa mwanzoni katika nia ya Mungu kiko sasa katika mwili wa Yesu Kristo. Yesu akifanya mapenzi na kanisa, Bibi Arusi wake, akimnong'oneza siri zake huyo bibi Arusi. Unajua vile ambavyo

unamzungumzia mke wako mambo, unajua msichana mdogo yule ambaye unaenda kumuo. Unampenda sana, unamwambia siri na kumfanya moyo wake akuandamie na kukupenda wewe na kila kitu. Unajua vile ilivyo. Hivyo ndivyo Kristo – Mungu anavyofanya kwa kanisa anamwachilia yeye ajue siri zile sio hawa viruka njia; namaanisha mke wake [1]

Sasa, kule kupigwa baragumu, mjumbe huyu, Malaika wa saba hapa, anapiga baragumu ya ujumbe wake kwa Kanisa la Laodikia (Ufunuo 3:11) Angalia aina ya ujumbe wake. Sasa, haukuwa kwa malaika wa kwanza (hakupewa huo), malaika wa pili, watatu, wanne, watano, wasita; lakini ni malaika wa saba ambaye ana ujumbe wa aina hii. Ilikuwa ni nini? Angalia, aina ya ujumbe wake; kumalizia siri zote za Mungu ambazo zimeandikwa katika kitabu. Malaika wa saba anazikusanya pamoja siri zote ambazo zilikuwa hazikuwekwa wazi, vyote kupitia haya madhehebu na vyama. Malaika wa saba anazikusanya zote na kuimaliza siri yote. Hivyo ndivyo ambavyo Biblia inasema kumaliza siri za kitabu kilichoandikwa. Malaika wa saba wa ufunuo 10:7 ni mjumbe wa wakati wa saba wa Kanisa [2]

Angalia siku ile hasa wakati huyu mjumbe, sio inapoanza juu ya, lakini anapoanza kutangaza ujumbe wake. Unaona? Mvuto wa kwanza uponyaji; mvuto wa pili, kutoa unabii; mvuto wa tatu, kule kufunguliwa kwa Neno, siri zinafunuliwa. Hakuna kiwango cha juu zaidi ya manabii katika kulifunua Neno. Lakini njia pekee ambayo nabii anaweza kuthibitishwa ni kwa njia ya Neno. Na kumbuka ule mvuto wa tatu wa kufunguliwa kwa ile mihuri saba, kufunua kweli zilizofichika ambazo zilitiwa muhuri katika Neno. Je unaliona hilo? Ni wakati huo, katika siku hizo mambo haya yanapotendeka ambapo Yanne na Yambre, waigizaji, watatokea tena, kama tu walivyofanya wakati Musa alipotokea na lile neno la asili (mwanzoni) akilina; wanatokea ili kuliigiza hilo, hiyo ni kweli kabisa, Sasa unaona kile Matayo 24:24 ilivyo? Unaona? Wapakwa mafuta. [3]

Sasa mjumbe huyu wa Malaki 4 na ufunuo 10:7 ataenda kufanya mambo mawili moja kulingana na Malaki 4 ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee Baba zao.

Mbili: Atafunua siri ya zile ngurumo saba za ufunuo 10 ambazo ni mafunuo yaliyo kwenye ile mihuri saba. Itakuwa ni kweli ya siri hizi zinapofunuliwa kiungu zinaigeuza hasa mioyo ya watoto kuwaelekea mababa wa Pentekoste (kitabu cha matendo) [4]

Lakini katika siku za mwisho inabidi iwe ni nabii ambaye anazichukuwa siri za Mungu, na kuzirudisha, kwa sababu siri hizo zilijulikana tu kwa manabii (Amosi 3:7)

Kwa hiyo itakuwa ni wakati huyu mtu ajapo, Unaona ninachomaanisha sasa? Hawezi akawa ni mtengenezaji; lazima awe ni Nabii, kwa sababu lazima awe mtu fulani ambaye ana vipawa karama na akae pale kuweza kujua lile Neno.

Sasa, watengenezaji walijua kuna kitu siyo sahihi. Luther alijua mkate ule haukuwa ni mwili wa Kristo nakadhalika, na hivyo alihubiri, “Mwenye haki ataishi kwa Imani” (Warumi 1:17) na huo ndio uliokuwa ujumbe wake.

Na wakati John Wesley alipokuja, aliona kuwa kuna utakaso, kwa hiyo alihubiri utakaso Waebr 10:10,14; Waebr 12:14) na huo ndio uliokuwa ujumbe wake.

Wapentekoste walileta ujumbe wa Roho Mtakatifu na kadhalika (Isaya 28:11-12; Matendo 2:1-21). Lakini katika siku za mwisho, katika wakati huu wa mwisho yule mjumbe hataanzisha matengenezo yoyote, lakini atachukua siri zote ambazo hawa watengenezaji waliyacha na atazikusanya pamoja na kuyaweka wazi mbele ya watu. [5].

Amefanya nini? Amefungua zile muhuri saba za ujumbe wa mwisho, uliona hilo? Mihuri saba, ambayo siri zote za nyakati saba za kanisa zilifungwa/zilitiwa mhuri na mihuri saba. Watengenezaji hawakuwa na muda kufanya hivyo katika wakati wao. Hawakuishi muda wa kutosha. Lakini ufunuo huu uliobarikiwa wa mihuri saba unafunguliwa kwetu katika siku hizi za mwisho kutokana na unabii uliotolewa wa kwenda Arizona [6].

Magazeti yaliichukuwa, wakaonyesha picha yake. Tukaja hapa na kuona siri zile kuu zilizofichika katika Biblia, zikafunguka kwetu kutupa uwanja mpya ambao hatujaujua kabla, na kuunganisha kikamilifu kule kuja kwa Bwana Yesu [7]

Oh, ndugu, dada, je unalipata hilo? Angalia Je huoni? Lilikuwa limefunikwa kupitia hizi nyakati kutokana na Mungu alivyosema, na itafunguliwa katika siku za mwisho; hiyo mihuri saba itavunjwa, na kitu chote kikamilifu kitaweza kuonekana na watu, kile kilichotokea katika wakati wote. Saa ya ujumbe wa malaika wa saba, siri zote za Mungu zitajulikana kupitia yule Eliya, katika saa hii ya mwisho: jinsi vile Kristo

alivyowekwa nje ya Kanisa kama mwana wa Mungu; jinsi anavyofunuliwa kama mwana wa Adamu tena; jinsi kanisa linavyowekwa katika utaratibu, na kila kitu katika siku za mwisho, na hakuna kanuni, hakuna dhehebu, ni lile Neno tu lenyewe likiishi ndani ya mtu binafsi. “Nitamtwa mmoja na kumwacha mmoja. “Nitamchukua huyu mmoja na kumuacha yule mmoja. “Nitamchukuwa huyu mmoja na kumuacha mmoja.” Hakuna kamba, hakuna dhehebu, hakuna cha kufunga au chochote; Ni ule moyo na Mungu na Yeye pekee. [8]

Sasa, hebu tuone chache ya hizo siri. Na kama unataka pia, ziandike chini kwanza, nitachukuwa kile Skofield alichosema Matayo 13

“Akajibu akawaambia, ninyi mmejaliwa....kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, lakini wao hawakujaliwa” (Siri).

Siri ni hii: Siri ni maandikoambayo “ni kweli zilizofichika, ambazo sasa zinafunuliwa kiungu, lakini bado kunabakia namna ya kiajabu pamoja na kufunuliwa huko” Siri zilizo kuu sana na siri zilizo kuu ni:

- 1.Siri ya ufalme wa Mbinguni ambayo ndiyo tunayozungumzia sasa,Mathayo 13:3-15
2. Sasa, siri ya pili ni siri ya upofu wa Israeli katika wakati huu: Rumi 11:25 pamoja na yaliyomo
3. Siri ya tatu ni siri ya kubadilishwa ya wakati wa mwisho: 1 Korith 15:51-58 na pia 1 Wathesalonike 4:14-17
4. Siri ya nne, kwamba kanisa la Agano jipya ni mwili mmoja, unaunganisha wote wawili wayahudi na watu wa mataifa: Waefeso 2:11-22, 3:1-11, Rumi 16:25-27, na pia Waefeso 6:19, Wakolosai 4:3
5. Siri ya tano ni ya Kanisa, kama Bibi Arusi wa Kristo: Waefeso 5:22-33.
6. Siri ya sita ni ya Kristo aishiye, Yeye yule jana, leo na hata milele. Wagalatia 2:19-21, na Waebr 13:8, na sehemu nyingi kama hizo.
7. Siri ya saba ni ya Mungu, ambaye ni Kristo, Mungu akikaa kwa utimilifu wote katika umbo la kibinadamu, ambaye kwa Yeye hekima yote ya Kimungu na uungu wote unarudishwa kwa wanadamu (Kolosai 1:27-29; 2:1-3, 9; Yohana 1:1-3, 14-18; 1Tim 3:16; Kolosai 2:9-10, 2Wakor 5:19)
8. Uzao wa nyoka, hiyo imekuwa siri iliyofichika katika miaka yote (Mwanzo 3:1-19; 2 Wakor 11:1-3; Matayo 13:24-30,36-39;Matayo 15:13;1Yoh 3:10-12)
9. Siri ya tisa ni siri ya uasi ipatikanayo katika 2 Wathesalonike 2:7-12 na kadhalika)
10. Siri ya kumi ni ile ya nyota saba za ufunuo 1:20 Nyota saba ni wajumbe saba wa makanisa saba na kadhalika

11. Na siri ya kumi na moja ni Babiloni ya siri, kahaba wa ufunuo 17:1-18 na 18:1-10. Hizo ni kati ya siri ambazo huyo Malaika anapaswa kuziweka wazi, siri zote za Mungu.....na hebu niseme hili kwa kicho, siyo kumaanisha mimi mwenyewe, lakini kwa kumaanisha yule malaika wa Mungu.
12. Neema ikinyooshwa, siyo neema iliyopotoshwa, lakini neema ya kweli. Hakuna kitu kama moto wa milele utaungua kwa mamilioni ya miaka, lakini chochote ambacho ni cha milele hakina Mwanzo wala mwisho, na kuzimu ilikuwa imeumbwa (Ufunuo 19:20;20:12-15)
13. Siri hizi zote kama wapakwa mafuta wa uongo na wakweli (Matayo 24:24;Matayo 5:45;Matayo 7:15-23)
14. Siri ya ubatizo wa Roho Mtakatifu bila msisimko. Lakini utu wa Kristo ukitenda ndani yako, kazi zilezile ambazo alizifanya (Waefeso 1:13-14;Matendo10:14-46)
15. Siri ya ubatizo wa maji (Matendo 2:38-41),ambapo watu walioenda mbali wa utatu wauleta katika vyeo vya Baba, mwana, Roho Mtakatifu, na siri ya uungu ikitimizwa katika ubatizo kwa jina la Yesu Kristo kutokana na kitabu cha ufunuo, ambacho kanisa lingepokea katika saa hii. Hizo ni baadhi ya siri.
16. Kurudi tena kwa nguzo ya moto (Matendo 22:6-11) hayo ndiyo yanayopaswa kutokea, nasi tunayaona. Oh, tunaweza kuendelea tu kutaja siri. Tunaiona ile nguzo ya moto iliyoongoza wana wa Israel, ile ile iliyomwangusha sauli njiani kwenda Damaskas. (Matendo 9:1-8).
- 8). Na yuleyule, alikuja na nguvu zilezile, akifanya mambo yaleyale, na akilifunua Neno lililele, akichukua Neno kwa neno na Biblia [2]

Hapa kuna siri zaidi zinafunuliwa:

17. Kule kutoka kwa tatu (kutoka kwa kwanza, kwa pili na kutoka kwa tatu, kutoka 3:1-22; matayo 4:12-17;Matayo5-7; Malaki 4:5-6;Ufunuo 10)
18. Kule kuzaliwa kwa pili (Roho wa Mungu akikubatiza wewe katika mwili wa Kristo – Maji, damu, roho, 1Yohana 5:6-8; Yohana3:1-8;1Cor12:13)
19. Uumbaji wake wa pili (Ufunuo 3:14;1Cor15:45-50)
20. Mtu mpya – mtu wa zamani (Efeso 2:11-17;4:20-24)
21. Warumi 7:1-6 kama unabii wa siku zetu kuokolewa tena katika wakati wetu na Kristo, Neno.
22. Siri ya kuunganika kati ya Bwana Arusi wa mbinguni na Bibi Arusi wake wa duniani – sasa hivi ni wakati wa kuungana (Waefeso 5:30-32)
23. Kule kufanywa wana katika sehemu tatu (Rum 8:15-16;Waefeso 1:5;Rum8:22-23)
24. Mpango wa wokovu-Damu tangu mwanzo (Mwanzo

- 3:21;Yohan1:29;Ufunuo 5:6).
25. Ndoa na talaka (Matayo 5:31-32;Matayo19:3-12)
26. Kujitambua sisi ni nani katika katika sehemu ya Mungu-mawazo ya milele ya Mungu – mbegu Neno/chembe ya Mungu – sasa inadhihirishwa (inaonekana) Yoh:17:6,16)
27. Tukiumbe mwenye sehemu tatu – Nafsi, roho, mwili na hisi (1 Thesalonike 5:23-24)
28. Nini maana ya uamsho leo: kujiweka kwenye mstari na Neno 2 Petro 1:12;-13) kwa Bibi Arusi leo (Warumi 12:2;Waefeso4:20-24)
29. Kule kugeuzwa/kubadilishwa kwa Bibi Arusi leo (Warumi 12:2;Waefeso 4:20-24)
30. Makao ya aina tatu ya kuishi: Mwili wa dunia/mwili wa mbinguni (theophany), mwili wa utukufu (2 Cor5:1;Filip3:20:2).
31. Maana ya kuhesabiwa haki – kamwe hujalifanya (Warumi 8:1-2)
32. Siri ya kuchaguliwa na kuteuliwa kimbele (Warumi 8:28-30;Wefeso1:3-5)
33. Ukamilifu ni ndani ya Kristo (Matayo 5:48;Waebr5:13-14;Waebr6:1- 3;Wafil3:15-16)
34. Ufufuko wa ndani naufufuko wa nje (ufufuko wa kwanza), au ukamilifu wa ufufuko (Waefeso 2:1-7;1Wathes4:16-17;ufunuo20:4-6)
35. Siri ya ngurumo saba za ufunuo 10:1-7 (Yohana 12:28-31)
36. Ile siri ya kuja kwa Bwana na unyakuo, kuja kwake kama mwana wa Adamu, mwana wa Mungu, katika siku zetu mwana wa Adamu tena, halafu kama Mwana wa Daudi (1Wathesalonike 4:13-17;Luke 17:30-36;Ufunuo1:7)
37. Siri ya mihuri saba na wapanda farasi wanne (ufunuo 6:1-17,8:1-5)
38. Siri ya mhuri wa sita – katika sehemu tatu (Ufunuo 6:12-17;Matay 24:29-3)
39. Siri ya mhuri wa saba – katika sehemu tatu (Ufunuo 8:1-5;Ufu10:Matayo 24:32-51)
40. Siri ya Israel wa kiroho wa Biblia (Imani ya Kiroho – mbegu ya Ibrahimu (Wagalatia 3:7-9,29;Wagal 6:16)
41. Siri ya Kristo – jinsi alivyokuwa kusudi la Mungu katika sehemu tatu ndani ya kanisa (Wakol 1:24-28;2Wakor 5:18-19)
42. Ile siri jinsi Kristo alivyotolewa nje ya kanisa lake kama mwana wa Mungu katika wakati wa kanisa wa Laodikia (Ufunuo 3:20-21)
43. Badiliko la wakati (Waefeso 1:9-10)
44. Vile viwango 7 – tunakwenda wapi baada ya kifo cha mwili? (Luka 16:19-31;Wafilipi 1:21-24;Yohan14:1-3)
45. Utawala wa miaka Elf – mbingu za kwanza – na nani atakuwa pale? (Isaya 65:17-25;Ufunuo 20:4;Ufunuo 21:1)
46. Ufufuko wa pili na hukumu ya kiti cheupe ufunuo 20:4-6,11-15).

47. Hali ya mwana mwali mwenye busara na mwanamwali mpumbavu (Matayo 25:1-13).
48. Kule kufanywa upya kwa dunia – Maji, damu na moto wa kiroho (2 Petro 3:1-15; ufunuo 21:1).L
49. Mbingu mpya na nchi mpya (2 Petro 3:11-13;ufunuo 21:1)
50. Yerusalemu ya mbinguni (Ufunuo 21:2-7,9-27; ufunuo 22:1-5)

Mungu ameyaficha machoni pa wenye hekima na akili na kuahidi kuyafunua kwa wana wa Mungu katika siku za mwisho, wakati wana wa Mungu watakapodhihirishwa (Warumi 8:18-23). Wakati wana wa Mungu walipofurahi pamoja naye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (Ayubu 38:1-7), wakati ufunuo mkuu wa uungu na mengineyo vitakapofunuliwa katika siku za mwisho, atadhihirisha mambo haya kwa wana wa Mungu unajua maandiko yanafundisha hivyo na tuko hapo hiyo ndiyo sababu Mungu anafungua haya mambo kwetu Mungu anawaleta watoto wake kwenye udhihirisho. Anaendelea na kuvuka upeo wa kiwango cha maarifa ya mwanadamu, mbali katika ufunuo wa kiroho na kuuleta kwetu.

Je hatukuwa tukifundisha juu ya Biblia? “Hapa ndio kwa huyo mwenye hekima na akili” Siyo kwa alichosoma chuo fulani cha seminary, lakini ni kile alichosoma magotini mbele za Mungu na kile kilichompendeza Mungu kumpa yeye. Wana wa Mungu wakidhihirishwa (Matayo 11:25-2) [9]

Ile siri ilikuwa katika mihuri saba wakati mihuri ile saba ilipofunguliwa, hiyo ilifungua Biblia yote. Ile mihuri saba, ilikuwa imefungwa na siri saba. Na katika hii mihuri saba, ilishikilia siri yote ya hayo, na ilikuwa ni kitabu cha ukombozi [10]

Neno lake ni mkate ilikuwa ni manna kamilifu, ambayo, kama mtu anaishi kwa hiyo hatakufa kamwe. Lakini baada ya vifo vya mababa, hakukuwa na hata mmoja aliyonekana kuelewa ukweli hasa na baada ya muda mfupi ile manna ilionekana ikiwa imefichwa kwa watu lakini katika kila wakati Mungu alianza kuuleta ufunuo ambao ulikuwa umefichika mpaka siku hizi za mwisho kulingana na ufunuo 10:7, Nabii atakuja na kufunua siri zote na baada ya hapo sasa Bwana atakuja. Sasa katika kila wakati, nasema wale wajumbe walipokea sio kwa ajili yao wenyewe tu. Lakini ilikuwa kama vile wanafunzi walipoombwa kugawanya mikate na samaki kwa makutano; Yesu aliwapa wao chakula kilichovunjwa na wao wakakigawanya na kuwapa watu. Mungu anawapa washindi maana yake iliyofichwa (Ufunuo

2:17). Haiwezi kuwa vinginevyo. Hawezi kuwafungulia hazina yake wale wanaopuza kile kilichofunuliwa tayari. [11]

Natwende kwa jina la Bwana Yesu Kristo, tukiinua bendera juu sana, na tukiwa na Imani katika Neno lake kuchukuwa upanga ukatao kiwili pamoja na ngao na silaha zote za Mungu pamoja nasi, tukapambane na adui, kwa sababu anaonekana kuongezeka nguvu na kuwa na uwezo kila siku kama adui ajavyo kama mafuriko, Roho wa Mungu atainua juu kiwango cha kumpinga Kama tumefika mwisho wa mambo haya kwamba tu na siri za Mungu zimekamiliwa kwetu, tunategemea nguvu zaidi, nguvu za kunyakuliwa kukutana na nguvu mbaya, ambayo italifanya kanisa linyakuliwe na kuchukuliwa utukufuni lakini tuwe nayo. Na tuendee mwaka huu mpya na himizo, kwamba sisi ni watumishi wa Mungu aliyehai. Na kama Shadrack, Meshaki na Abednego wa zamani, hatutapiga goti kwa mashetani wa dunia hii na huvikanusha vitu hivi tulivyovizungumzia juu yake, badala yake tukaze mwendo vitani [12]

Ninaomba Baba, kwamba watatambua kuwa siyo kulaani walicho nacho; ni kujaribu tu kuwapa Neema zaidi ya kunyakuliwa kwa maana saa inakuja ni lazima tuwe na nguvu ya kunyakuliwa, siyo tu ya kuponya mwili ila kuubadilisha katika muda mfupi kufumba na kufumbua jicho. Kristo atakuwa halisi sana katika miili yao, kiasi kwamba anaweza kuibadilisha kwa nguvu yake kuu ya mauti na ya kile alichokinunua. Hebu waichukue hii leo, ile Ishara niliyoizungumzia usiku wa jana, waishikilie mbele yao na watembe kuelekea huyu mwana anga (Jalia hilo Baba), ambapo maono, nguvu na dunia zilizo mbali na zijulikanazo, na Ee Mungu, mahali ambapo siri kuu zote za Mungu zimefunguliwa/zimewekwa wazi katika mihuri hii saba na kujulikana miongoni mwa watu. Jalia hilo Baba [13]

Nukuu za Kiingereza

- [1] “Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa” uk 58
- [2] “je mabwana hii ndiyo ishara ya mwisho” (62-1230e) uk 30-32
- [3] “Wapakwa mafuta wa siku za mwisho”, Aya 262
- [4] “Wakati wa kanisa la Laodikia” Nyakati za kanisa uk 327
- [5] “Muhuri wa kwanza kitabu cha mihuri” uk 145
- [6] “Muungano usioonekana wa Bibi Arusi” uk 28
- [7] “kutaharuki” (Desperation) Aya 52
- [8] “Kufunuliwa kwa Uungu” Aya 184
- [9] “Uzao wa nyoka” uk 21-22
- [10] “Roho zilizoko kifungoni sasa” uk 24
- [11] “Wakati wa kanisa la Pergamo” Ni nyakati za kanisa uk 210
- [12] “Lile shindano” (62-1231) Aya 33
- [13] “ Kuhesabu kinyume nyume” (64-0209) Aya 93

Jiwe la kiroho la kujengea na 162 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii yamekusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, D-753228 Schomberg, Germany, simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia, Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo na utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E.Y. Kanju
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@Hotmail.com
cellphone: 0784 704299*